**HALMASHAURI YA KIJIJI CHA VIANZI- MKAMBA**

OFISI YA MTENDAJI KIJIJI,
KIJIJI CHA VIANZI,
KATA YA KISEGESE ,
S.L.P 165,
MKURANGA,
07/11/2016.

KUMB. NO. HK/VIA/VL/BR/DED/VOL. 1/016/02,

MHE.
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 10,
MKURANGA.

**YAH: MAOMBI YA HUDUMA YA USHAURI JUU YA MAUZAJI NA MANUNUZI YA SHAMBA**

MHE. somo la hapo juu kama linavyosema,

Kufuatia tangazo lako katika vyombo vya habari ambalo ulitoa mnamo mwezi August 2016, la kuepuka migogoro ya ardhi kutokana na uuzwaji holela wa viwanja na mashamba.

Ofisi yangu imepokea barua kutoka kwa kampuni ya Rubis, iliyopo Dar es salaam, ambayo imetutambulisha na kuomba ridhaa ya kununua shamba lenye ukubwa hekari 100 ndani ya kijiji cha vianzi kwa lengo la shughuli za kilimo.
Kampuni hiyo inatarajia kununua eneo hilo kutoka kwa mzee HOSSENI SAIDI UPINDE mkazi wa hapa Vianzi. Maelezo mafupi ni kwamba maeneo hayo yapo na ni mali ya mzee HUSSEN S. UPINDE na hayana mgogoro wowote.
Na muuzaji yupo tayari kuuza eneo lake na mnunuzi yupo tayari kulinunua eneo husika.

Hivyo ninaomba ushauri ili kuweza kufanikisha jambo hilo.
Pamoja na barua hii nimeambatanisha na nakala ya barua ya kampuni ya RUBIS.

Nakutakia kazi njema.

..........................................
NDANDE S. I
VEO- VIANZI
0657- 072572

AFISA MTENDAJI
KIJIJI CHA VIANZ
S. L. P 165 MKURANGA

**NAKALA**
WEO- KISEGESE- kwa taarifa.